**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Kuchunguza Sababu Zinazowalazimu Wahusika Kufanya Ukahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema Na Ndoto ya Almasi

*Karuhanga Deusdedit[1*] & Prof. Florence Ngesa Indede, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Maseno, S. L. P. 3275-40100, Kisumu, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: karuhangad1@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*01 Mei 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Ukahaba, Ngono, Kuwadi, Madanguro.*

**IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza suala la ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema (Mohamed S.Mohamed) na Ndoto ya Almasi (Ken Walibora)*. Kitendo cha ukahaba kimesababisha mashaka mengi sana katika maisha ya mwanadamu kama vile kupoteza ujira, uharibikaji wa ndoa, maradhi ya zinaa, vifo, kukata tamaa na utengano miongoni mwa wanajamii. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni: kubainisha usawiri wa ukahaba na wahusika makahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi*; kuchunguza sababu zinazowalazimu wahusika kufanya ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi*; na kudhihirisha athari za ukahaba kwa wahusika waliomo katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi*. Mtafiti alitumia nadharia ya utekelezi ambayo ni miongoni mwa nadharia nyingi zenye mtazamo wa kisosholojia. Nadharia ya utekelezi imeendelezwa na wanasosholojia kama vile Talcort Parsons na Emile Durkheim kama wanavyonukuliwa na Worsely Introducing Sociology (1970), huku akisema kwamba ukahaba husababishwa na mambo mawili yaani haja ya kutekeleza mahitaji ya kiuchumi na kwa kukidhi matashi ya nafsi zao kiashki. Mtafiti pia alitumia nadharia ya umaksi iliyoanzishwa na Karl Marx (1818-1863) na Fredrich Engles(1820-1895). Nadharia hii hufaa utafiti huu kwa kudhihirisha wahusika wanaoshiriki katika vitendo vya ukahaba kwa ajili ya kupata fedha au zawadi. Mabepari au walionacho huwa na lengo la kuridhisha miili yao tu na wanyonge huwa na lengo la kupata pesa ili kutimiza mahitaji yao, pengine, mnyonge hutolea mwili wake kwa ajili ya kupewa kazi au kupandishwa cheo kazini au kama njia ya kuilinda kazi yake ili asipigwe kalamu. Utafiti huu ni wa maktabani kwa hivyo, maktaba yaliyotumika ni yale ya Chuo Kikuu cha uislamu kilichopo nchini Uganda, Chuo kikuu cha Bishop Stuart Mbarara, na maktabani ya shule ya upili Heritage. Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka maktabani kwa kutumia

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

mbinu ya usomaji makini na uchunguzaji wa riwaya teule yaani: ile ya *Nyota ya Rehema* na ya *Ndoto ya Almasi* kwa kuzisoma na kuzichambua kwa kina na kuiwasilishwa data kwa mbinu ya kiuthamano. Utafiti huu umebainisha kuwa wahusika hufanya ukahaba ili kupata pesa au kuridhisha matashi ya nafsi zao kiashiki. Utafiti huu utakuwa wa muhimu sana kwa kufunza jamii kwamba kahaba si mwanamke peke yake kama inavyochukuliwa katika baadhi ya jamii bali kahaba ni mtu yeyote awe mwanamume au mwanamke anayeshiririki vitendo vya uzinzi.

**APA CITATION**

Deusdedit, K. & Indede, F. N. (2023). Kuchunguza Sababu Zinazowalazimu Wahusika Kufanya Ukahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema Na Ndoto ya Almasi *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 119-131. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194.

**CHICAGO CITATION**

Deusdedit, Karuhanga and Florence Ngesa Indede. 2023. "Kuchunguza Sababu Zinazowalazimu Wahusika Kufanya Ukahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema Na Ndoto ya Almasi". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 119-131. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194.

**HARVARD CITATION**

Deusdedit, K. & Indede, F. N. (2023) "Kuchunguza Sababu Zinazowalazimu Wahusika Kufanya Ukahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema Na Ndoto ya Almasi", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 119-131. doi: 10.37284/jammk.6.1.1194.

**IEEE CITATION**

K. Deusdedit & F. N. Indede, "Kuchunguza Sababu Zinazowalazimu Wahusika Kufanya Ukahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema Na Ndoto ya Almasi", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 119-131, May. 2023.

**MLA CITATION**

Deusdedit, Karuhanga & Florence Ngesa Indede. "Kuchunguza Sababu Zinazowalazimu Wahusika Kufanya Ukahaba katika Riwaya ya Nyota ya Rehema Na Ndoto ya Almasi". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, May. 2023, pp. 119-131, doi:10.37284/jammk.6.1.1194.

## UTANGULIZI

### Usuli wa Mada

Kitendo cha ukahaba chaweza kufasiliwa kama mwenendo wa mwanaume na mwanamke kushiriki katika kitendo cha ngono kama biashara au kwa kukidhi matashi, ukahaba, uasherati, uzinifu, na uzinzi (TUKI, 2004). Riwaya nyingi za Kiswahili zilizoandikwa baada ya uhuru na kuendelea hadi hii leo zinalenga kujenga jamii mpya kwa kuielimisha, kuikosoa, kuionya na kwa kiasi fulani kuiburudisha (Nguma, 2001).

Kulingana na Mbilinyi (1983, uk.14-16), mwanamke alikuwa akichukuliwa kama chanzo cha utafiti barani Afrika kuanzia miaka ya sitini na sabini kipindi cha kupigania uhuru kwa nchi nyingi za Afrika. Nyanja mbalimbali za serikali zilihamasishwa kuanza utafiti kuhusu mwanamke, idadi kubwa ya wanawake iliyokuwa ikijihusisha na ukahaba, wasichana wengi kupata mimba, na wengine kukimbilia mjini kisha ukahaba ukaongezeka miongoni mwa wanawake na wasichana katika vichochoro vya miji.

Suala la ukahaba lina uhusiano mkubwa na unyonge, Bakwesigha (1982, uk.11).Unyonge katika muktadha huu unamaanisha udhaifu wa nafsi na udhaifu wa elimu. Ilhali, ukahaba ni uhitaji wa kifedha na kukidhi matashi ya nafsi (mapenzi yasiyojali ndoa). Kuna unyonge unaosababishwa na kupoteza au kutengwa na walezi, hali hii huleta fedheha kwa taswira ya malezi mabaya ambapo talaka nyingi hutokea, ndoa huvunjika na mara nyingi husababisha unyonge wa nafsi na kiuchumi. Kwa hiyo, kazi hii iliangazia jinsi unyonge unavyowalemaza wahusika wengi mpaka wakajiingiza katika vitendo vya ukahaba. Katika mantiki hii, kuna swali, je! Mwanamke ndiye

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

kahaba peke yake au mwanamume pia ni kahaba? Wataalam mbalimbali wametoa suluhisho la swali hili kama vile; Waniston Dictionary (1948), hufasiri kahaba kama; mwanamke au mwanamme anayeshiriki mambo ya uzinifu au uzinzi au uasherati kwa lengo la kupata fedha.

Kishtainy na wenzake (1982, uk.32) wanaeleza kuwa, kahaba ni mwanamke au mwanamme anayeshiriki mapenzi ya watu wengi kwa matarajio ya pesa au zawadi bila kuwa na hisia za mapenzi ya dhati. Pia wengine hufanya ukahaba kwa ajili ya kuridhisha nafsi zao kiashiki. Katika muktadha huu, ni muhimu tubainishe mambo yanayomtambulisha kahaba, kuna uthibitisho kwamba kahaba awe wa kike au wa kiume, daima hutolea mwili wake kwa ajii ya mapato au kitu kingine. Kulingana na mtazamo wa elimu nafsi, washiriki ukahaba kwa kawaida huwa na lengo la kuridhisha nafsi zenye kiu cha mapenzi. Hivyo, mtazamo huu unathibitisha kwamba, katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi* wahusika wanaume na wanawake kama msingi wa kuendeleza ukahaba, mtafiti hawezi kuwawekea mipaka wahusika makahaba mbali na jinsi walivyosawiriwa na wasanii wa riwaya hizi mbili yaani ya Ken Walibora na Mohammad S. Mohammad. Makahaba tunaopata katika mamadanguro wakiuza miili yao kwa minajili ya kujipatia fedha ili wapate kuendesha masiha yao; hili ndilo tabaka la chini katika taasisi za ukahaba; kuna kundi lingine ambalo kwalo hukaribishana au kuamkiana kwa miili yao ya uke na uume kutagusaana, wengine hutumia miili yao kuwashawishi mabosi kuwaajiri, kupandishwa cheo kazini au kuongezwa mshahara kwa mfano tunamwangalia mhusika Rehema anavyoogopa kufanya ukahaba na bosi wake Bwana Mansuri lakini kwa ajili ya kazi, hapo basi hatimaye akakubali .(uk63). Hawa hawapatikani katika madanguro bali hupatikana katika nyanja fulani za maisha kama vile viwandani na kampuni mbalimbali.

Vijana wa kike na kiumehuuza miili yao kwa mabibi na mabwana wakwasi ili wapate kutimiza mahitaji yao katika maisha, na kwa upande wa wakwasi hawa huwa na hitaji la kutagusana kimwili na vibarubaru sio kwa lengo la pesa kama hao bali ni kwa lengo la kukidhi utashi tu. Pesa zao huwafanyia kama mtego wa kuwanasia vibarubaru hawa kama vyombo vya kusherehekea kingono. Mtafiti akizungumzia kuhusu mapenzi mara nyingi anamaanisha mahaba aliyonayo mtu juu ya mtu mwingine au kitu. Saumu Juma Khamis(2017),Kama itakayofafanuliwa hapo baadaye kwamba mapenzi hugawanyika katika pande mbili; ambazo ni mapenzi ya dhati na mapenzi ya bandia. Mapenzi ya dhati siku zote hujenga utulivu, umoja, amani na usawa miongoni mwa watu wanaoishi katika eneo moja na wenye masilahi yanayofanana ilhari, mapenzi ya bandia huzaa chuki na uhasama miongoni mwa wanajamii kwa hiyo mapenzi ya bandia ndicho kiini cha migogoro, mitafuruku, na uozo wa hisia za umoja na hatimaye mtu huishia akiichukia familia au jamii yake. (Nguma, 2001).

**Suala la Utafiti**

Kitendo cha ukahaba kimesababisha mashaka mengi sana katika maisha ya mwanadamu kama vile kufutwa kazini, uharibikaji wa ndoa, maradhi ya zinaa, vifo, kukata tamaa pamoja na utengano miongoni mwa wanajamii. Katika kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili, suala la ukahaba limejitokeza mara kadhaa wa kadhaa, pale ambapo wasanii huwasawiri baadhi ya wahusika wao kama Makahaba pamoja na kudhihirisha uwanja wa shida zinazowakabili. Hiyo, kukaonekana haja ya kufanya utafiti wa kina katika fasihi ya kiswahili hususani utanzu wa riwaya kuhusu ukahaba. Kwa kadri ya uelewa wa mtafiti, licha ya jitihada za tafiti zilizotangulia hazikuchunguza na kufafanua kwa undani suala la ukahaba katika riwaya ya Kiswahili, kwa hiyo, mtafiti aliteua riwaya ya ***Nyota ya Rehema*** **na*****Ndoto ya Almasi*** ili kulichunguza kwa kina suala hili na kubainisha jinsi wasanii wanavyowasawiri wahusika wao kama Makahaba, sababu zinazowasukuma kufanya ukahaba na athari zinazowapata wahusika hawa katika shughuli za

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

utendaji wa ngono. Hizi riwaya zimechaguliwa kwa sababu ndani yake maudhui ya ukahaba yanajitokeza mara nyingi pale ambapo watunzi huwachora baadhi ya wahusika waliomo namna wanavyojihusisha na kitendo cha ukahaba kama tegemeo lao linalowafanikisha katika maisha ya wenye uhai. Hili ndilo pengo la kitaaluma ambalo mtafiti alikusudia kuliziba, na katika mchakato huo, utafiti huu ulichunguza usawiri wa suala la ukahaba katika riwaya ya ***Nyota ya Rehema*****na*****Ndoto ya Almasi***.

**Madhumuni ya Utafiti**

- Kuchunguza sababu zinazowalazimu wahusika kufanya ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi*.

**Maswali ya Utafiti**

- Ni sababu zipi zinazowalazimu wahusika kufanya ukahaba katika Riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi*?

**Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti ulikuwa wa muhimu mkubwa katika uwanja wa fasihi kwa kuchunguza kwa mapana na marefu suala la ukahaba katika riwaya za Kiswahili *Nyota ya Rehemana Ndoto ya Almasi*kama zilizochaguliwa miongoni mwa nyinginezo. Pia, kwa wasomi utawapa mwelekeo na uelewa jinsi ya kuchanganua maswala ya ukahaba kitaalumaUtafiti huu utasawiri dhamira ya ukahaba inayowasilishwa katika riwaya hizi kwa waandishi hawa tofouti. Zaidi ya hayo, utafiti huu utakuwa dira na mwongozo kwa watafiti wa baadaye watakaochunguza zaidi kuhusu suala ka ukahaba katika tanzu mbalimbali za fasihi. Wahusika makahaba katika kazi za fasihi hutumulikia kuona ukandamizaji unaojitokeza katika jamii, maana hapo tunapata kujua hali zetu na hali za ulimwengu unaotuzunguka.

Utafiti huu utakuwa wa umuhimu kwa wanawake ili kuwatia hamasa kujitahidi na kufanya kazi zilizo halali ili waepukane na hadhi ya umaskini inayowalazimu kujishughulisha na matendo ya ukahaba ambayo ni hatari kwa afya yao. Utafiti huu utawaelimisha wanawake wote jinsi ya kuchunga nafsi zao na kupata elimu.Utafiti huu utaelimisha wanafunzi kuhusu tabia zinazosababisha mtu kuwa kahaba ili waweze kuepukana nazo.

Utafiti huu una mchango mkubwa katika taaluma ya fasihi na utunzi wa riwaya za Kiswahili hususani kwa jamii ya Wanauganda. Kwanza, unatoa mchango wa kubainisha usawiri wa suala la ukahaba katika riwaya za Kiswahili; *Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi*. Utafiti umeweza kuwaweka bayana wahusika wanaojihusisha na ukahaba katika riwaya hizi. Pili, utafiti huu umeweza kubainisha sababu zinazowafanya wavulana na wasichana kujihusisha na vitendo vya ukahaba katika Riwaya. Tatu, utafiti huu unachangia kuonyesha athari hasi za ukahaba zinazoweza kujitokeza kwa wahusika wanaojishughulisha na suala hili katika jamii na athari zinazoweza kuikabili jamii kwa kuwemo wahusika wakahaba.

## NADHARIA ZA UTAFITI

TUKI (2004) wanafasili nadharia kuwa ni dira, mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kufafanua, kutatua au kutekeleza jambo fulani. Nao, Wafula na Njogu (2007), wanaeleza kuwa nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza mtu wakati wa kusoma kazi ya fasihi na kuifahamu katika vipengele vyake vyote. Wataalamu hawa wanaendelea kufafanua kwamba nadharia ni maelezo ya jambo kufungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyoibuka kutokana na majaribio ya jambo hilo. Mdee na wenzake (2011)wanaeleza kuwa nadharia ni mpango wa mawazo yaliotungwa ili kuongoza na kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Jilala (2016)anaifasili nadharia kuwa ni wazo ambalo huzuka kama dira kwa msomaji ama mchambuzi na hali mwanafasihi alivyolinganisha katika kutoa majumulisho ya kazi za fasihi na zisizo

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

za fasihi. Kutokana na fasili hizo tunaweza kusema kwamba nadharia ni kigezo kinachotumika kumwelekeza mtu katika kuchunguza au kutathmini jambo fulani. Kwa kuwa ukahaba ni suala lenye mawanda mapana sana, nadharia moja haitoshi kulitatathmini bali mtafiti aliona heri kutumia nadharia mbili yaani nadharia ya umaksi na ya utekelezi ili kulitathmini kiukamilifu. Hii ni kwa sababu ukahaba husababishwa na hali mbalimbali za kiuchumi, kisaikolojia, na kisosiolojia.

### Nadharia ya Umaksi

Nadharia hii ilianzishwa na Karl Marx (1818-1863) na Fredrich Engles (1820-1895). Nadharia hii inachangia kwa kudadavua na kuelezea juu ya hadhi za tabaka mbalimbali katika jamii na hali ya maisha ya wanadamu waliyomo. Katika nadharia hii, Marx amejikita katika historia na miundo ya kijamii kwa kupitia hoja kuu tatu zifuatazo: Historia ya maisha ya mwanadamu yaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo inachunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi pia huathiri uzalishaji mali na usambazaji wa mali hizo. Hivi vyote kwa pamoja huunda misingi ambapo kwenye misingi hiyo huunda maadili, itikadi, dini na utamaduni. Hoja nyingine ni kuamini kuwa historia ya binadamu inadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi jamii. Marx alisema “Historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka katika jamii” (Mwandawiro Mghanga, 1997.Nadharia ya Kimaksi inaangalia matabaka katika ngazi mbalimbali kama vile ngazi ya familia, dini na elimu. Ubepari kama njia ya uzalishaji mali na mara nyingi huathiriwa na tabaka la chini hivyo ubepari hujitengenezea njia za kujiharibu wenyewe kutokana na unyonyaji na ukandamizaji unaotendeka kwa tabaka la chini. Mabepari hawa au walionacho kulingana na Marx ni tabaka la wale ambao wana uwezo wa kununua nguvu za wengine na wenye mali wakazalisha mali zaidi. Anaendelea kusema kuwa wasionacho ni lile kundi la watu ambao huuza nguvu zao kwa mamwinyi na kipato wanachokipata mara nyingi huwa hakiwatoshi. Matabaka mbalimbali husababishwa na mali, siyo kipato tu. Marx anandelea kusema kuwa walionacho huendelea kuwanyonya wasionacho na kuwalipa kipato kinachotosha kununua chakula na kulipia makazi yao, na wafanyakazi wanaoshindwa kuelewa kuwa wananyonywa huchukulia kusema kuwa wao wako afadhali. Nadharia hii hufaa utafiti huu kwa kudhihirisha wahusika wanaoshiriki katika vitendo vya ukahaba kwa lengo la kupata fedha au zawadi. Mabepari au walionacho huwa na lengo la kuridhisha matashi ya nafsi zao kiashki na wanyonge huwa na lengo la kupata pesa ili kutimiza mahitaji yao, pengine, mnyonge hutolea mwili wake kwa lengo la kupewa kazi au kupandishwa cheo kazini au kama njia ya kuilinda kazi yake ili asipoteze ujira. Hapa tunavumbua kwamba tabaka la chini katika jamii hukandamizwa na tabaka la juu kwa kuwa mnyonge huwa anataka kupata riziki na kwa hiyo hana hiari yoyote bali kumtegemea bepari maana ndiye mwenye jibu la mashaka yake kwake. Kulingana na msimamo wa nadharia hii, wanadamu katika jamii hushiriki na kujiunga na taasisi za ukahaba sio kwa hiari yao bali kwa madhumuni ya kupata fedha ili waepukane na hadhi ya unyonge lakini wanachopewa huwa hakitoshi na kwa hiyo huendeleza shughuli za ukahaba kama kazi yao rasmi ya kuwapa riziki. Nadhari ya umaksi haijitoshelezi peke yake kwa hivyo nadharia ya utekelezi ilitumika pia ili kuelezea suala la wahusika kufanya ukahana ili kukidhi miili yao.

### Nadharia ya Utekelezi

Nadharia ya utekelezi imejengeka katika misingi ya elimu jamii (Lowry, 1974, uk.198). Nadharia hii huzungumzia juu ya mtazamo wa kisosholojia. Nadharia hii imeendelezwa sana na wanasosholojia kama vile Talcort Parsons na Emile Durkheim kama wanavyonukuliwa na Worsely (1970). Wanasoshiolojia hawa husisitiza kwamba nadharia ya utekelezi hujishughulisha sana na jukumu linalotekelezwa na taasisi mbalimbali za jamii kwa madhumuni ya maendeleo ya jamii. Hii ni nadharia yenye mtazamo wa kisosholojia yaani inahusisha muktadha wa jamii na muundo wake. Kulingana na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

mtazamo wa kifasihi, nadharia ya utekelezi huandamana na nadharia ya miundo. Peck na Coyle katika kazi yao *How to study literature, litercìry terms and criticisms* (1984) wanasema nadharia ya utekelezi na miundo ni "ndugu" kwani hujikita katika ufafanuzi wa instilahi za jamii kama mfumo mmoja uliogawanyika katika viungo vingi vinavyofanya kazi kwa pamoja. Kila kiungo kina nafasi na dhima ya kuchangia na kutekeleza katika jamii. Nadharia hizi zote mbili hutathimini uhakiki wa kazi mbalimbali za kifasihi zenye mwelekeo fulani, usawiri wa wahusika, na uchambuzi wa kazi ya msanii kwa jumla. Nadharia hii ya kisosholojia ina mtazamo kwarnba ukahaba husababishwa na hali ya kiuchumi pamoja na hali ya kuridhisha matashi ya nafsi zao kiashki yaani hali ya mhusika fulani kutaka kutimiza mahitaji ya kifedha au kuridhisha nafsi ni uhitaji na uhitaji hauwezi ukapimika. Maana matajiri huwa na uhitaji wao sawa na maskini. Hivyo nadharia hii inafaa katika kuelezea ni kwa nini waanawake na wanaume matajiri hushiriki katika ukahaba sawa na wafanyavyo mahohe hahe.

Kingsley David ambaye amenukuliwa na Lowry, ni mwanasosholojia mwenye mtazamo wa kiutekelezi-amenukuliwa. Mawazo yake yamejikita sana katika ufafanuzi wa masuala ya kijamii (Lowry, 1974, uk.220). David ananukuliwa akieleza kwamba katika jamii ya kisasa, kuna sababu kadha wa kadha zinazofafanua kuwepo kwa suala la ukahaba. Kwanza, ukahaba husababishwa na ile haja ya kutaka kunufaisha hadhi ya kiuchumi pamoja na mahitaji ya kuridhisha miili. Kingsley, anaendelea kusema kuwa mapenzi huuzwa katika miktadha mbalimba1i ya kijamii hasa katika ndoa, usuria, na katika mashindano ya urembo. Hata hivyo miktadha hii haijahesabika kama ukahaba, maana viwango vya matumizi yake ni tofauti.

Davis anaendelea kudai kwamba ukahaba ni taasisi inayohusiana sana na taasisi nyingine kama vile ndoa na kadhalika(Lowry, 1974,uk.224). Watu wengi ambao hawaridhiki na ndoa zao agha1abu hupata mapenzi nje ya ndoa kupitia ukahaba: "Katika jamii za kisasa, wanawake na wanaume hujihusisha katika vitendo vya ukahaba kama njia ya pekee ya kutosheleza kiu cha mapenzi walichonacho yaani kuridhisha nafsi pamoja na kujinufaisha kiuchumi. Mwenendo huu huchangia pakubwa katika kuboresha hali ya wenye ndoa zisizokamilika". (Utafsiri wa mtafiti). Kulingana na dondoo hili, jamii ina viungo vingi 1akini vinauhusiana sana na ukahaba na ndoa. Hivyo basi, ukahaba huteke1eza mambo makuu mawili katika jamii yaani kutimiza mapato ya kifedha na matashi ya nafsi zao kimwi1i ambayo hayawezi kuteke1ezwa na taasisi nyingine katika jamii hata ndoa. Kwa hivyo ni heri kuhitimisha kwamba, mbali na athari hasi ziliomo, taasisi ya ukahaba humsaidia mwanamume na mwanamke katika ndoa yao. Kwa mfano tunamwangalia mhusika Chemtai mke wa pili wa mzee Kirwa ambaye anafanya ukahaba na kila mwanamume ili kupata mtoto, anazaa watoto saba na kila mtoto ana baba yake kutoka kabila tofouti. *Ndoto ya Almasi* (uk 47): Kulingana na jamii inayowasilishwa na Ken Walibora katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi*, mwanamke akiwa tasa huruhusiwa kumwoa mke mwingine ili amzalie watoto mumewe. Chemtai anapokutana na Almasi hapo mtoni kapteriti, kwa utashi zaidi wa kuridhisha nafsi za mwili wake, anamshawishi na hatimaye wanazama katika dimbwi la mapenzi hapo kwa hapo. Ukahaba hutuliza moyo wa mtu ili apate kufanya shughuli zake za kawaida lakini mtu huyu akikosa kuuridhisha mwili huu wenye kiuutashi zaidi wa mwili kiashki, hawezi akatulia hata kamwe *Nyota ya Rehema*. *(uk 63)*.

Mtazamo wake Kingsley (Lowry, 1974,uk.120), huwashtumu wale wataalamu wenye mtazamo wa kimaadili wanaodai kwamba ukahaba ni dhambi na ni uhuni, na wanasayansi wanaodai kuwa ukahaba husababisha maradhi na kwa hivyo unastahili kukomeshwa, Kingsley, anasema kuwa ukahaba hausababishi maradhi ila tu maradhi husababishwa na ujinga kuhusu mapenzi na matumizi ya mapenzi holelaholela.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

Maoni ya Davis na wenzake, Finnegan (1979) na Muga (1980) wana upacha kimtazamo ambapo wote hudai kwamba jamii za kisasa huhitaji huduma za ukahaba kama huduma nyinginezo. Wanaosiolojia hawa wanadai kuwa jamii huwa na viungo mbali mbali vya kazi vile walimu, wanajeshi, madereva, maafisa fulani, wanasiasa, wafanyabiashara, na manahodha. Watu hawa wote huwa na mahitaji ya huduma kutoka kwa makahaba ili kuridhisha miili yao. Isitoshe, nadharia ya utekelezi hushikilia kwamba taasisi ya ukahaba ni hali ya kimaisha inayosababishwa na hali ya kutaka kunufaisha mahitaji ya uchumi wa jamii pamoja na ile hali ya kutaka kuridhisha utashi wa nafsi ya mtu husika. Ukahaba hauwezi kuondolewa katika jamii isipokuwa jamii ikiweka mikakati na mabadiliko yatakayoruhusu njia halali za mapato ya kiuchumi pamoja na kudumisha ndoa zilizojengwa kwenye misingi ya amani, usawa, ukamilifu na uaminifu. Nadharia hii hutoa ufafanuzi mkubwa kuhusu taasisi ya ukahaba. Ni dhahiri kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya ndoa na ukahaba ambapo zote ni taasisi zinazotegemeana kwa njia mbalimbali. Maana wanawake au wanaume huweza kutoka katika taasisi moja na kujiunga na taasisi nyingine miongoni mwa hizi mbili, hivyo basi, ndoa kama imedadavuliwa hapo juu huamilishwa na ukahaba.

## MBINU ZA UTAFITI

### Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kiuthamano, ulitumia mbinu ya usomaji makini na uchunguzaji wa riwaya teule yaani: riwaya ya *Nyota ya Rehema* na riwaya ya *Ndoto ya Almasi*. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kuzihakiki riwaya hizi mbili kwa kutumia na kuongozwa na msingi wa nadharia ya utekelezi na umaksi.

### Uteuzi wa Sampuli

Kothari (2004) anaeleza kuwa sampuli ni kikundi fulani cha vitu au watu kilichomo ndani ya mkusanyiko wa watu ambacho mtafiti anaamini kwamba kikundi hicho kitampatia taarifa anayohitaji kuhusu utafiti wake. Kwa sababu hiyo, mtafiti hulazimika kuteua kitu fulani au watu ambao huitwa kundi lengwa. Kwa hiyo katika utafiti huu, mtafiti alitumia riwaya ya *Nyota ya Rehema na* riwaya ya*Ndoto ya Almasi* kwa sababu riwaya hizi zimebeba uwanja wa vipengele vya ukahaba ambavyo mtafiti alikusudia kuvichunguza kwa kina kwa kuangalizia wahusika wanaoshughulika na vitendo vya ukahaba, sababu zinazowaletea kufanya ukahaba, na athari zinazowapata.

### Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Scale (2012) na Silver (2010)wanasema kwamba zipo mbinu mbalimbali za kukusanya data na katika mbinu hizo hakuna mbinu inayojitosheleza katika mazingira yake. Mbinu ya usomaji matini kwa kusoma vitabu teule, riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi*ilitumiwa. Data ilikusanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti. Pia tasnifu zenye uhusiano na mada ya mtafiti zilisomwa kwa makini.

### Mbinu ya Maktaba

Kothari (2004) anaelezea mbinu hii kuwa ni mbinu inayohusisha uchambuzi wa maudhui yaliyomo katika nyaraka kama vile vitabu, tahakiki, magazeti, majarida, na vitabu vya ziada kulingana na malengo ya utafiti ili kupata data zilizokidhi haja ya kiutafiti pamoja na maudhui ya maneno ambayo yanaweza kuwa ya maandishi au mazungumzo. Sababu ya kuchagua kutumia mbinu hii ni kwamba inafahamika kuwa tafsiri huwa katika matini mbili zilizoandikwa (rej. Cartford, 1965; Newmark, 1981 na Mwansoko 1996). Nao Pyne & Weber (2007) wanasema kuwa matini hutoa taarifa za awali. Kwa maana hiyo, matini andishi ndiyo chanzo kikuu cha data ya tafsiri. Katika utafiti huu, matini andishi ndiyo ilikuwa chanzo kikuu cha data. Kwa hiyo uchanganuzi huu ulifanywa kwa kutumia mbinu ya maelezo. Data zilizokusanywa kutoka riwaya ziliteuliwa na kupangwa ili zichambuliwe kwa urahisi. Uchunguzi huu wa kina uliwezesha mtafiti kuhakiki kwa makini vipengele vya ukahaba

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

vinavyojitokeza katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi* na jinsi vinavyosaidia kuwasawiri wahusika kama makahaba.

### Vifaa vya Ukusanyaji wa Data

TUKI (2004) wanafasili data kuwa ni taarifa au takwimu ambayo hutumiwa kuelezea au kuthibitisha hoja fulani. Vifaa vya kukusanyia data ni vifaa mbalimbali ambavyo hutumika katika kukusanya na kuhifadhi data za utafiti. Katika harakati za kukusanya data za utafiti huu, mtafiti alitumia vifaa mbalimbali kama; shajara na kumpyuta mpakato.

#### *Kompyuta Mpakato*

Kompyuta ni mashine ya kielektroniki ya kuhifadhi na kuchanganua taarifa zilizoingizwa, kukokotolea na kuongoza mitambo. Pia, kwa upande wa kompyuta pakatwa, hii ni aina ya kompyuta inayoweza kubebeka kwa urahisi kutoka sehemu moja hadi nyingine ambayo huweza kupakatwa. Katika utafiti huu, kompyuta pakatwa ilimsaidia mtafiti wakati wa kuandaa pendekezo la utafiti, kuhifadhi data zilizokusanywa, kuhifadhi data na kuandika ripoti ya utafiti. Aidha, kalamu na karatasi ni vifaa vya asili katika ukusanyaji wa data ya utafiti. Bila shaka vifaa hivi vitaendelea kutumika kwa miaka mingi ijayo. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia daftari na kalamu ambavyo vilimsaidia katika kuhifadhi kumbukumbu za uchanganuzi wa ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi*.

### Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa Omar (2009) uchambuzi wa data ni mbinu inayomruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma kazi ya fasihi kwa lengo la kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo na kadhalika. Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo ilisaidia kujibu maswali ya utafiti unaohusika. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo katika kuchanganua data za utafiti kwa kuwa data za utafiti huu zilikusanywa kwa mkabala usio wa kiidadi, pia uchambuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kiuthamano. Kutokana na hali hiyo data zilizokusanywa kutoka riywaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi* ziliwekwa katika makundi na kisha kuwasilishwa ili kuweza kufikia malengo mahsusi ya utafiti huu.

## UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

### Riwaya ya Nyota ya Rehema

Riwaya ya *Nyota ya Rehema* iliandikwa na Mohamed S. Mohamed mwaka 1976. Mohamed Sulaiman Mohamed alizaliwa tarehe 5 octoba 1943 kijijini Koani katika sehemu ya kati ya kisiwa cha Unguja. Riwaya hii imejikita katika mapenzi na ukahaba. Imeakisi mandhari ya kisiwa cha Unguja huko Zanzibar. Ina sura kumi na moja kwa utaratibu vizuri ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Dhamira kuu ya riwaya hii ni kutakasa na kukosoa jamii iliyokwamia katika shughuli za ukahaba, kukata tamaa na kuoza kimaadili ili iweze kupambazuka na kuchomoza kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni, kuepukana hali ya unyonge. Mohamed Sulaiman Mohamed anasawiri wahusika wake kama makahaba wanaoshiriki ukahaba kwa ajili ya kupata pesa, Mohamed anazingatia sana kipengele cha ukahaba wa kupata fedha bora kuliko ule wa kuridhisha nafsi kwa hiyo nadharia ya umaksi iliyotumiwa na mtafiti inaifa kazi hii kiuhakiki.

### Riwaya ya Ndoto ya Almasi

Riwaya ya *Ndoto ya Almasi* iliandikwa na Ken Walibora, mwaka 2006 na imejikita katika kuonyesha hali ya misukosuko ya maisha yanayomkabili mhusika mkuu wa riwaya hii aitwaye Almasi. Riwaya hii imeakisi mandhari ya usasa ambapo ina sura kumi na tatu zilizopangiliwa vizuri ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Dhamira kuu ya riwaya hii ni kudhihirisha vikwamizi vya maisha vinavyomkumba mwanadamu na kumkataza kutimiza ndoto yake katika maisha na vikwamizi hivi vinajikita katika kipengele cha

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

mtindo wa kisasa, utamaduni, na masuala ya kijamii kama vile ndoa, mapenzi, na kazi. Ken Walibora amewasawiri wahusika wake kama makahaba kwa kuzingatia kipengele cha kukidhi nafsi badala ya kupata fedha kwa hiyo, nadharia ya utekelezi imeifaa kazi hii kiuhakiki.

**Sababu za Ukahaba katika Riwaya na Jamii**

Sehemu hii inajadili na kufafanua lengo mahususi la pili ambalo lilitaka kuchunguza sababu za ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi.* Kwa mujibu wa utafiti huu, inaonekana kuwa katika jamii zinazoakisiwa na waandishi, kuna watu wengi ambao wanalipinga suala la ukahaba. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kufanya ukahaba ni tendo la aibu na fedheha linalolaaniwa na watu wa imani za dini mbalimbali. Hivyo, mwanamke au mwanamume anayejishughualisha na ukahaba anaonekana kama aliyekosa malezi na maadili mema katika familia yake.

Kwa kutumia mbinu ya maktaba, yaani usomaji na uchambuzi wa makala, majarida, tafiti za wali, magazeti, hadithi fupi, riwaya na tamthilia, utafiti huu ulichunguza sababu kadhaa wa kadha ambazo huchangia pakubwa katika usababishi wa ukahaba. Uchanganuzi wa sababu hizi umeongozwa na nadharia ya utekelezi ambayo mtafiti ameiteua kuitumia katika utafiti huu. Hivyobasi, uchanganuzi na usomaji wa kazi za kifasihi zilizotambuliwa hapo juu, mtafiti amepata sababu zifuatazo zinazowalazimu wanawake na wanaume kushiriki vitendo vya ukahaba. Kwanza kabisa, kuna uchu zaidi ya mapenzi; Kulingana na kazi za kifasihi, mtafiti amevumbua kwamba kimaumbile kuna watu ambao wana uchu zaidi ya mapenzi. Watu kama hawa hutoka kwenye familia ambazo si imala, walikosa mapenzi ya wazazi na kwa hiyo wakikua huwa wanataka kulipiza kisasi yaani kugusia mapenzi yale yale waliyoyakosa utotoni. Katika harakati za kutimiza utashi huu wa maisha. Mfano riwaya ya Ndoto ya Almasi (Uk 47):, huishia wameraruliwararuliwa na mafisi dume wanayojifunika ngozi ya kondoo kumbe ni fisi makahaba. Hapo basi, wakijikuta kiasi kwamba maji yamezidi unga, huamua kuedeleza na kujinyakulia hadhi ya juu katika ukahaba kama kazi ya kawaida ambayo inasababisha kipato cha kila siku na wahusika hawana aibu ya kuendeleza ukahaba maana wamekizoea kitendo hiki kama kazi ya kawaida. (Uk 46 ).

Kwa nafano tunamwangalia mhusika Rehema katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* (uk 74) . Yeye alifikiri kwamba hatua ya Bwana Mansuri kumnunulia nguo ilikuwa ya mapenzi ya dhati au kwamba ilikuwa imesindikizwa na roho ya uzazi kumbe njama ilikuwa ya kumtega mtego wa kumnasia na kumwangusha katika pakacha la ngono au ukahaba. Baada ya Rehema kufutwa kazini, kaamua kuujimwaga katika taasisi ya ukahaba kirasmi na marafiki zake akina Ruzuna, Chiku, na Kidawa. (Uk 47 )

Pili, tamaa ya utajiri. Kuna baadhi ya wanawake hunafanya mapenzi na wanaume wasio waume zao ambao wana uwezo wa kifedha kwa tamaa ya kupata mali kama vile kujengewa nyumba, kununuliwa magari na mengineyo. Pia, wanawake wengi hufanya mapenzi ili waweze kupandishwa vyeo kazini na wengine hufanya ukahaba ili kupata kazi. Sababu hii inabainishwa kupitia mhusika Rehema katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, katika harakati zake za kufanya ukahaba na bwana Mansuri hakuwa na mapenzi ya dhati bali tunamwona akitekemeka ishara ya “nifanye?? sifanye??” lakini hisia za kuhifadhi kazi zilipompamba kama moto wa kiangazi msituni, basi akaamua kufanya kitendo cha ukahaba (uk. 74).

Tatu, baadhi ya wanawake hujiingiza taasisi za ukahaba kwa kukata tamaa. Mohamed Sulaimana Mohamed alithiriwa na mwelekeo wa falsafa ya kukata tama katika usawiri wa mhusika Rehema. Falsafa hii ya kukata tamaa imeendelezwa vizuri na mwandishi mashuhuri wa Algeria aitwaye Albert camus (Cruickshank: 1958, uk.27), anaposema; ‘Maisha ya binadamu akiwa hapa duniani huwa

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

yamepangwa kwa sababu ya kimaumbile na kwa amri ya Mungu na anaweza kuyabadilisha. Kwa kudhibiti dondoo hili, twaona jukumu linalotekelezwa na jamaa katika malezi ya Rehema jijini Ramwe na maisha yalivyobadilika yakawa magumu wakati alipoanza kuishi na mama'ake wa kambo Bi-Adila. Hivyo basi, Rehema akaamua kutoroka nyumbani huku akifikiri kuwa maisha yatakuwa afadhaliuk 2 Wasichana na wavulana wengi hutoroka vijijini na kuelekea mijini kwa lengo la kutafuta uhuru na haki ambazo wamenyimwa na wazazi wao au mabwana zao kama asemavyo Little (1973, uk.22). Wakifika mjini, hukuta kuwa mambo ni kinyume na vile walivyokuwa wakifikiri na hapo basi huamua kujiingiza ukahaba.

Uharibikaji wa ndoa husababisha ukahaba. Mohamed Sulaimani Mohamed anamsawiri mhusika Chiku kama mwanamke anayeshiriki ukahaba baada ya ndoa yake kuharibika. Fasihi huwa inaakisi yale yanayojitokeza katika jamii, mwandishi hapa anaonesha kwamba wanawake na wanaume wengi wanaopatikana katika taasisi za ukahaba vichochoroni mjini ni wale wale waliokuwa wamefunga ndoa zikaharibika. Watu kama hawa huwa wamezoea ngono, na kwa hivyo hawawezi kuishi bila kushiriki vitendo vya ngono, pia huwa wamekuwa wanawategemea mabwana zao kiuchumi lakini sasa ni kujitegemea wenyewe.( Carrie A. Miles, 2012)Vigezo hivi vyote viwili huwa lazimu kushiriki taasisi za ukahaba. Isitoshe, husukumwa na hisia na utashi wa kuridhisha nafsi za kiashki. Matajiri wengi hushiriki ukahaba ili kuridhisha utashi wa miili yao maana hawana mapenzi ya dhati isipokuwa huishi maisha ya nipa nikupe yaani kununua wale wanyonge wasio na pesa, wafanye nao ukahaba na baadaye wawatupe kama ganda la ndizi. Mohamed Sulaiman Mohamed anadhihirisha vile Fuad anavyomtupa Bi Aziza baada ya kumwoa mke mpya Bi Adila.(uk14). Kuna hata wale wa tabaka la chini ambao hawanunui ngono kwa sababu ya utashi wa pesa, lakini nao kimaumbile hushiriki ukahaba ili kuridhisha matashi ya nafsi zao (Mhilu na wenzake, 2013)

Mwanndishi Ken Wlibora katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* anadhihirisha wahusika wake wakishiriki ukahaba kwa ajili ya kuridhisha matashi ya yao kimwili wala sio kwa mahitaji ya fedha. Wahusika hawa ni: Chemtai na Almasi (uk. 47,68-69), Chebosio na Almasi (uk. 28, 52 na 140-145), Nakhumicha (uk. 21 na 52). Kuna wanawake na wanaume ambao hujiingiza katika ukahaba kwa ajili ya kujistarehesha tu. Hapa kuna wanawake wa aina mbili; kuna wale wanawake wasio na waume na wana uchu zaidi wa kufanya ngono ili kuridhisha utashi wa mwili. Pia kuna wanawake wenye wanaume na wana imani kufanya ukahaba na wanaume wa nje ya ndoa kama mmojawapo wa njia ya kuhifadhi ndoa kwa sababu waume zao hawawaridhishi kiasi cha kutosha yaani ni wadhhaifu wa ngono. Hawa ni wanawake ambao wanajihisi kutotosheka kimapenzi kwa waume zao wa ndoa. Sababu hii haikuoneshwa kwa upande wa wahusika wanawake katika riwaya teule zote mbili. Baali kwa upande wa wanaume takribani wote wanafanya ukahaba kwa lengo la kutuliza kiu cha miili yao kuhusu mapenzi. Hayo tunayaona kupitia wahusika kama vile Mansuri katika riwaya ya *Nyota ya Rehema*, Mzee Masasi, Almasi katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi*.

Kuna wanawake ambao huifanyia biashara miili yao kwa kufanya ukahaba na watu wasio waume zao kwa ajili ya kupata mahitaji yao ya kila siku kama manukato, chakula, mavazi, na malazi bora. Hawa ni wale wanawake maskini ambao huitumia miili yao kama kitega uchumi cha kujipatia mahitaji. Baadhi ya wanawake wa kundi hili hujikuta wanafanya ukahaba katika maisha yao ya kila siku. Sababu hiyo inadhihirika katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* kupitia mhusika Chiku na Ruzuna. Hawa walitoka nyumbani kwao wakaja mjini Topea kwa ajili ya kuuza miili yao kama biashara yao ya kuwazidishia mapato, maana wasipoifanya hawatapata chakula wala nguo au mahitaji yanayowafaa kuishi. Pia, kuna wanaume ambao

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

wapo katika ndoa ambao hutoka nje ya ndoa zao kwa kutembea na wanawake wasio wake zao kwa ajili ya kupata watoto. Hawa ni wale wanaume wanaogundua kwamba wake zao wa ndoa ni tasa yaani wana matatizo ya mfumo wa uzazi kiasi ambacho hawana uwezo wa kuzaa.(Rose Nancy lowrence,2015). Hivyo wanaume au wanawake hao hutoka nje ya ndoa zao kutafuta watoto. Sababu hii mwandishiKen Walibora anaidadavua katika riwaya ya *Ndoto ya Almasi* pale ambapo mke wa pili wa mzee Kirwa alikuwa tasa na kulingana na mila na desturi za kwao, mke akiwa tasa hapo basi mke huyo mwenyewe ambaye ni tasa ana uhuru wa kumwoa mke ili apate kumzalia watoto mumewe. Hapa suala la ukahaba linajitokeza pale ambapo Chemtai ambaye ni mke wa mke wa pili wa mzee Kirwa baadala ya kumzalia watoto Kirwa, anaamua kufanya ukahaba na wanaume wengine hapo mwanzoni, akaamua kuwagawia mapenzi wanaume na bila kuwabagua kisura,rangi au kabila kama inavyofafanuliwa katika riwaya. (Uk 47)

Kuna wanawake ambao hujiingiza katika ukahaba baada ya kubakwa. Hawa ni wale wanawake ambao hulazimishwa kufanya ngono kwa nguvu au bila ridhaa zao. Miongoni mwa sababu za kubakwa zilizobainishwa ni pamoja na kuwa na sura nzuri, kutembea nusu uchi, na kukalia kulipa fadhila kwa wanaume waliowasaidia jambo fulani. Mwandishi wa riwaya ya *Nyota ya Rehema* ameionyesha sababu hii pale Bwana Mansuri anapomtamani hivi mara ya kwanza Rehema anapofika kwake. Hapo anapitia awamu ya kwanza kumshawishi kwa kosa alilofanya, Rehema anapokuja kumwomba msamaha hapo basi dume lile likamnyosha mkono na kumwingiza bila ridhaa yake Rehema (uk.80). Hatimaye, sababu zilizotolewa hapo juu ni zile ambazo mtafiti alipata kutoka kwa riwaya ya *Nyota ya Rehema* na *Ndoto ya Almasi* pamoja na kazi nyingine za kifasihi kama vile Majarida, hadithi fupi, magazeti na tasnifu za tafiti tangulizi alizopata fulsa ya kuzisoma kwa umakilifu hodari, kuzichunguza kwa kina. Tunaweza kusema kuwa waandishi wa riwaya hizi hawakulipa uzito unaostahili suala la ukahaba. Pengine waliliona halina athari kubwa katika jamii yao likilinganishwa na suala la harakati za ujenzi wa jamii mpya. Kwa ujumla, nadharia ya utekelezi imemsaidia mtafiti kuchambua sababu za ukahaba zilizobainishwa katika riwaya teule.

## HITIMISHO

Utafiti huu ulichunguza ukahaba katika riwaya mbili za Kiswahili ambazo ni riwaya za *Nyota ya Rehema*na *Ndoto ya Almasi*. Lengo kuu ni kuangalia usawiri wa suala hili katika riwaya zilizoteuliwa yaani jinsi waandishi wa kazi hizi za kifasihi wanavyosawiri suala la ukahaba na msimamo wao. Kwa hakika kipengele hiki cha kulinganisha suala la ukahaba katika riwaya hizi mbili, tafiti zilizotangulia zilijikwepa. Utafiti huu umebainisha kuwa usawiri wa ukahaba katika riwaya ya *Nyoya ya Rehema na Ndoto ya Almasi*ni tofauti kulingana na jinsi waandishi walivyolisawiri suala hili kimtazamo. Katika riwaya zote mbili, waandishi wanawachora baadhi ya wahusika wakiwahusisha na vitendo vya ukahaba lakini hawaoneshi kwa kina athari zinazowapata wanajamii na msimamo wa jamii kuhusu suala hili. Katika *Riwaya ya Nyota ya Rehema* mwandishi anamuonesha mhusika Rehema akifanya ukahaba na Bwana Mansuri, Bi Rose alipopata fununu kuwa mumewe anafanya ukahaba na yaya, akaamua kumfukuza yaya huyo ambaye ni Rehema. Lakini mwandishi Mohamed Sulaiman Mohamed hatuonyeshi athari zilizoipata ndoa ya Bi Rose na Mansuri hapo baadaye. Vilevile, katika *Riwaya ya Nd oto ya Almasi*, mwandishi anamuonesha mhusika Chemtai akijihusisha na ukahaba kwa kufanya mapenzi na wanaume mbalimbali hata wa kabila tofouti, watoto aliokuwa nao walikuwa wa mababa tofouti lakini haoneshi matatizo yaliyomkabili mhusika huyu Chemtai katika matendo yake ya ukahaba na ikiwa; je! aliendelea kuwatunza watoto hao yeye mwenyewe au aliwatunza na msada kutoka kwa baba zao? alitalakwa na mke wa pili wa mzee Kirwa au kasamehewa?.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

Kwa sababu hiyo, ni wazi kuwa waandishi wa *Riwaya ya Nyota ya Rehema*na *Ndoto ya Almasi* hawakufafanuakwa kina ukahaba kwa kudhihirisha athari zote zinazoweza kuwapata hata vijana na wanajamii wengine wanaojishughulisha na utendaji wa ukahaba. Ukosefu wa kufafanua kwa kina suala la ukahaba na athari zote ziliomo, huacha pengo la kutowapa wasomaji mafunzo kamili kuhusu suala la ukahaba maana kwamba wasomaji hawatapata faida hasi na chanya kuhusu kahaba.

**Mapendekezo**

Utafiti huu ulichunguza suala la ukahaba katika riwaya ya *Nyota ya Rehema na Ndoto ya Almasi*. Kwa hakika, hakuna utafiti ambao unaweza kuchukuliwa kuwa umekamilisha suala husika katika mada ya utafiti. Hivyo basi, ni wazi kwamba utafiti huu haukudadavuliwa na kutosheleza ukahaba katika utanzu wa riwaya ya Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti zaidi unahitajika kuchunguza ukahaba katika kazi nyingine za fasihi kama vile; Ngano, mashairi/ nyimbo, hadithi fupi na tamthilia. Halikadhalika utafiti wa ziada unaweza kufanywa kwa kuzingatia kipengere cha uchambuzi linganishi wa suala la ukahaba katika kazi ya kifasihi yoyote na uhalisia wake katika jamii.

**MAREJELEO**


Bakwesegha, C. (1982). *Profiles of Urban Prostitution:A case study from Uganda.*Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Bakwesigha(1982, uk.11). Relationship between sexuality and Poverty in Kampala Uganda

(Cruickshank: 1958, uk.27),

Carrie A. Miles, ( 2012) Tasnifu ya Ph.D . Mafundisho ya Biblia, Kuhusu Ndoa, Familia na Jinsia Swahili(Kenya)

Finnegan, F. (1979). *Poverty and Prostitution*

Ken. Walobora. (2006).*Ndoto ya Almasi*.(Moran East Africa publishers Limited

Kishtainy, K. (1982).*The Prostitute in Progressive Aliterature.* Alalinson and Busby Ltd:

Kothari, C. R. (2004).*Research Methodology: Methods and Techniques.* New Age International (P). New Delhi India.

Little, K. (1973). *Taswira ya mwanamke mjini.* Fasihi ya kiafrika. Cambridge University Press.

Lowry, R.P. (1974).*Social Problems*: *A Critical Analysis of Theories and Public Policy.*

Mbilinyi, M. (1983).*Mwanamke wa Tanzania:Analytical Bibliography*.Motala Crafisika, Sweden.

Mghanga, Uppsala, (1997) Demokrasi na Harakati za Kitabaka

Mohamed, M.S. (1972), KIU. (East African Publishing House). (1976). *Nyota ya Rehema*. (Oxford University Press).

Muga, E. (1980).*Studies in Prostitution: East, West and South Africa, Zaire and Naveda*. Kenya Literature Bureau: Nairobi.

Nguma, N. (2001), Taswira ya Mwanamke Jinsi Ilivyochorwa Katika Riwaya ya Kezilahabi. *Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

Omar, S. (2009), *Tanzania Hip Hop Poetry as Popular Literature*. (Tasnifu ya uzamili, haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Peck, J.,& Coyle, M. (1984).*How to study Literature, Literary terms and criticisms.*Macmillan Limited.

Rose Nancy lowrence(20215). Uchungu wa kujifungua nchini Tanzania

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1194

TUKI (2004).*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press

Karl Marx (1818-1863) na Fredrich Engles (1820-1895).Theory,beliefs and communism Manifesto

*Mdee na wenzake, (2011) Kuendelea kuwa wabunge hadi mahakama itakaposikiliza na kuamua*

Mwandawiro Mghanga, Uppsala, (1997 Demokrasi na Harakati za Kitabaka

Rose Nancy lowrence(20215). Uchungu wa kujifungua nchini Tanzania

Wafula na Njogu (2007), Nadharia za uhakiki wa Fasihi Jomo Kenyatta Foundation.

Worsely (1970). *The Three Worlds: Culture and World Development*. Pinguine Books, Ltd.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.